# SALAMU ZA MHE. HAMZA S. JOHARI MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MLEZI WA CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA KITAIFA LA SHERIA
## 21 JUNI 2025

---

- **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni wetu Rasmi;**
- **Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.) Naibu Waziri wa Katiba na Sheria;**
- **Mhe. Cosato Chumi (Mb.) Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;**
- **Mhe. Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro, Naibu Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa;**
- **Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;**
- **Ndugu Bavoo Junus, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania;**
- **Ndugu Viongozi wote wa Serikali mliopo hapa;**
- **Viongozi wote wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania;**

- **Mawakili wote wa Serikali na wa kujitegemea mliopo hapa;**
- **Viongozi wa Dini;**
- **Wageni waalikwa;**
- **Wanahabari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA! KAZI IENDELEE**

**ASKARI WA KALAMU! NDANI YA CHAMA KIKUBWA**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Nami niungane na wazungumzaji waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha sote kuhudhuria katika Kongamano hili. Aidha, na kwa upekee, nikushukuru sana Mhe. Mgeni Rasmi kwa kukubali mwaliko wetu, pamoja na ratiba ngumu ulizonazo. Tunakushukuru sana.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Kama ilivyoelezwa na Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Kongamano hili lina lengo la kujenga na kukuza uelewa wa Wananchi na Watanzania kwa ujumla kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria yanayohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Hii inatokana na mabadiliko ya mfumo wa kisheria yaliyofanyika mwaka jana 2024 ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria mbili muhimu ambazo ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 na Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Kutokana na umuhimu mkubwa wa sheria hizo mbili, kupitia katika Kongamano hili Wananchi na Watanzania kwa ujumla watapata fursa nzuri ya kupata uelewa kuhusu mfumo huo mpya wa kisheria kupitia Mada zitakazowasilishwa na Wanasheria wabobevu, lakini pia kupitia majadiliano na mijadala kuhusu

mifumo hiyo ya kisheria. Vilevile, Wananchi na Watanzania watapata nafasi ya kuuliza maswali kuhusiana na mada zitakazowasilishwa na kujadili kwa kina mfumo huo mpya wa kisheria kwa kuzingatia maudhui na maboresho yaliyofanyika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

Ni matarajio yetu kwamba Wananchi na Watanzania kwa ujumla watatumia kikamilifu fursa hii kujifunza na kujenga uelewa kuhusu mifumo yetu ya kisheria na hivyo kujiandaa kikamilifu kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi;**

**KWA HESHIMA NA TAADHIMA, NAOMBA SASA NIKUKARIBISHE UJE UONGEE NA HADHARA HII NA KUTOA HOTUBA YAKO. KARIBU SANA.**